# MASOMO YA BIBLIA


KWA

WATOTO WA MIAKA 4-6

## MWALIMU

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Kwanza



MSAIDIZI NAKUWA Key F
(A HELPER I WILL BE)

| | |
|---|---|
| Msaidizi na kuwa, | /:s d :- :d/d- :- - :d/ |
| Msaidizi na kuwa; | /m :- :m m :- :m/m :- :- :- ;m/ |
| Tu na kazi, | /s :- :s/s :- :ls :- :m/d :- :-/ |
| Tu na kazi, | /m :- :m/r :- :r/d :- :-/:- :-/ |
| Ndani kanisani. | |

MUNGU YU KARIBU Key B
(GOD IS VERY NEAR)

| | |
|---|---|
| Mungu Yu karibu, | /s :m d :l/t :t - :s/:f/ |
| Mungu Yu karibu; | /r :t/d :d ; :d/ |
| Hutusikia tunapo imba na kuomba, | /d :/t :l s :m/m :-/l :l/ |
| Mungu Yu karibu. | /t :s d/ :d -://  |

NAJUA MUNGU ANANITUNZA
(GOD TAKES CARE OF ME I KNOW).

Najua Mungu Ananitunza,
Mchana, na Usiku,
Najua Mungu Ananitunza,
Mungu Ananitunza.

Key F /s :- :m/r :d :r/m :- :f/:m :m :-/
/s :- :m/r :- :-/s :m :m/:m ;- ;-/
/s :- :m/r :d :r/m :m :f/m :m :-/
/r :m :f/m :- :r/d :- :-/- :- :-//

OH, HOW I LOVE JESUS Key F

Oh, how I love Jesus,
Oh, how I love Jesus,
Oh, how I love Jesus,
Because He first loved me.

/m: -: /m :r :m /d :- :- /d :- :-
/r :- :- /r :d :r /m :- :- /s :- :f



# MASOMO YA BIBLIA

KWA

# WATOTO WA MIAKA 4-6

## MWALIMU

**Mwaka wa Pili** **Kitabu cha Kwanza**

B2 - 1Ts

Used by permission of International Publications Services

© Copyright, 1986
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

## HATUA ZA KUFUATA KATIKA KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Hatua ya 1: Jitayarishe mwenyewe kwa maombi.

Hatua ya 2: Soma somo lote.

Hatua ya 3: Soma kuhusu mkazo wa somo na ufikirie jinsi unaweza kutimiza lengo hilo.

Hatua ya 4: Soma maandiko ya Biblia.

Hatua ya 5: Jifunze kusimulia hadithi kwa watoto.

Hatua ya 6: Jifunze kifungu cha Kukumbuka.

Hatua ya 7: Jifunze kuimba nyimbo zilizopendekezwa.

Hatua ya 8: Jifunze mpango wa kufundisha somo.

Hatua ya 9: Fika mapema Jumapili na utayarishe mahali pa kukutania.

## HATUA ZA KUFUATA DARASANI MWAKO KILA JUMAPILI

Hatua ya 1: Fika mapema; na utayarishe mahali pa kukutania.

Hatua ya 2: Watoto wanapofika:
Mkaribishe kila mmoja, na umwite kwa jina lake.
Pokea sadaka.
Weka alama kwa kitabu cha rekodi.
Andika kila jina la mtoto katika kitabu.

Hatua ya 3: Kulifundisha somo:
Kila siku utatumia nyimbo, wakati wa maombi, vifungu vya Biblia, anza kusimulia hadithi ya Biblia kwa kitendo. Hata hivyo, utaratibu huu waweza kutofautiana; fuata mpango uliopendekezwa kila wiki.

Kila mara wape watoto nafasi ya kujibu maswali unayouliza na kushirikiana katika mawazo yao.

Hatua ya 4: Wakati watoto wanapoondoka:

Ikiwezekana, mpe kila mtoto karatasi ya kupeleka nyumbani ambayo ina picha ya hadithi ya leo.

DOKEZO: Kama watoto hawafahamu nyimbo zote, wafundishe wimbo mpya kila mwezi. Pia, waweza kutumia nyimbo wanazofahamu.

## JINSI YA KUFUNDISHA WIMBO MPYA

1. Imba wimbo wenyewe vizuri na pole pole huku watoto wakiwa wanasikiliza.
2. Baada ya kuuimba tena, waulize watoto una maana gani.
3. Waambie watoto waseme maneno yake baada ya kuyasema.
4. Waambie watoto waimbe pamoja nawe.
5. Rudia wimbo huo huo wakati tofauti mkiwa darasani.
6. Kumbuka kwamba utafundisha maneno yake, sauti na maana yake.

## JESUS HELPED THE SICK

Key F

| | |
|---|---|
| Jesus helped the sick, | /m .m :m .f /s :- / |
| Jesus helped the blind; | /r .r :r .m /f :- / |
| Every day he went about | /m .m :s .s /f .f :l / |
| Doing something kind. | /s .m :r .m /d :- // |

## YESU ANIPENDA (JESUS LOVES ME)

Key $E^b$

| | |
|---|---|
| Yesu Anipenda, | /s :m :s :s / .d' :-/s :m |
| Yesu Anipenda, | :d :d/m.r :-l |
| Kweli Anipenda, | /s :m :s :s l/.d' :- .l/s .d |
| Mungu Amesema. | :m/.r/d :-// |

## JESUS LOVES THE LITTLE CHILDREN OF THE WORLD

Jesus loves the little children,
All the children of the world.
Red and yellow, black and white,
They are precious in his sight;
Jesus loves the little children of the world.

## NJIA YA FURAHA (THE HAPPY WAY)

Na mpendaane,
Na mpendaane,
Hii ni njia ya Furaha,
Na mpendaane.

Na mshirikiane,
Na mshirikiane,
Hii ni njia ya furaha,
Na mshirikiane.

Na msaidiane,
Na msaidiane,
Hii ni njia ya furaha,
Na msaidiane.

Key D

/m .m :m .m/m :d/s .s :s .s/l :s,
/d' :t.l / s .l :s .f/m .m :s .m,
/r :d//

## NAWEZA KUKUA (I CAN GROW)

Ninafuraha kujua naweza kukua,
Sijui ni kwa nini?
Mama husema Mungu amepanga hivyo,
Ananitaka niwe mkubwa pia.

Key F

s d:d r:r m:f s f m'd r:t t d:l,
s d:d r:r m:f s:f m:m r:r d:-l-

## NYIMBO

### NISAIDIE KUWA MWEMA
### (HELP ME TO BE KIND)

Nisaidie kuwa mwema,
Ee Mungu siku yote;
Nisaidie kufanya yale yanipasayo,
Kazini kwangu na michezoni.

```
Key E^b   /s .s :l .s/s .f :m/r :d .r/m :-/
          /s .s :l .s/s .f :m/r .r :m .r/d :-/
```

### LEO TUNAFURAHA
### (WE'RE GLAD TODAY)

Twa furahi leo, twa furahi leo,
Kwa mama zetu twa furahi:
Asante Baba Mungu.

```
Key A^b
/s /m' :- :d /l :- :s /f' :- :t /l :- :- /
   /s :- :l /t :l :s /d' :- :r /m' :- :- /
   /l :- :- /d' :- :- /t :- :- /r' :- :- /
   /r' :- :- /- :- :- /d' :- :- /:- :- /
```

Tumia pia: baba, nyumba, chakula, na kadhalika.

### MARAFIKI
### (FRIENDS)

Marafiki, marafiki,
Sisi tu marafiki,
Kwa kucheza kwa furaha.

```
Key D
/s :l /s .m :d . /
/r .m :f .s /l .t :d' . /
```

### NAPENDA KANISA
### (I LIKE TO GO TO CHURCH)

```
Key G
: .s,d.r:m.f s:-.s d.r:m.f s:-.3
: f.m:r.f m.f:s.l s.f:m.r d:_.
```

Na-penda Ka-ni-sa,
Na-penda Ka-ni-sa,
Na-penda Ka-ni-sa,
Na-penda Nyi-mbo twa-im-ba,
Na-penda Ka-ni-sa.

### JUMAPILI YENYE FURAHA
### (HAPPY SUNDAY MORNING)

Jumapili yenye furaha,
Jumapili yenye furaha,
Husoma Biblia, kuimba na kuomba,
Asubuji hii njema.

```
Key E^b
/m .m :m .f /s :d' /
/l .l :t .l /s :m .s /
/f .m :r .f /m .l :s /
/d' .s :m .f /r :d //
```



## YALIYOMO

Hatua za kufuata katika kujitayarisha kufundisha ........ 2
Hatua za kufuata kila Jumapili darasani mwako ........ 2

### LENGO LA 1: WASHIRIKI WA KANISA NI RAFIKI ZANGU

**Kusudi:** Kumsaidia kila mwanafunzi kujua kwamba Mungu alimpangia awe na rafiki, na pia washiriki wa kanisa ni rafiki zake.

Kumsaidia kila mwanafunzi kujua kwamba anaweza kuonyeshwa upendo, naye pia anatakiwa aonyeshe upendo kwa wenzake.

Somo la 53 Marafiki wa Paulo Kanisani ........ 4
Somo la 54 Samweli na Eli ........ 6
Somo la 55 Ujenzi wa Kanisa ........ 8
Somo la 56 Msaada kwa Marafiki ........ 10

### LENGO LA 2: TWAJIFUNZA UPENDO WA MUNGU

**Kusudi:** Kumsaidia kila mtoto kujua kwamba Mungu anampenda.

Kumsaidia kila mtoto kujisikia kuwa anatunzwa kwa sababu Mungu anampenda na humtimizia mahitaji yake.

Somo la 57 Filipo Ashuhudia Upendo wa Mungu ........ 12
Somo la 58 Ndoto ya Yakobo ........ 14
Somo la 59 Daudi na Yonathani ........ 16
Somo la 60 Dorkasi, Msaidizi Mwema ........ 18
Somo la 61 Jamaa ya Mtoto Musa ........ 20

### LENGO LA 3: TWAJIFUNZA KUONYESHA UPENDO WA MUNGU

**Kusudi:** Kumsaidia kila mtoto ili atambue njia ambazo anaweza kuonyesha upendo wa Mungu.

Kumsaidia kila mtoto ili atambue njia ambazo anaweza kuonyesha upendo wake kwa wenzake.

Somo la 62 Yesu Akutana na Mwanamke Kisimani ........ 22
Somo la 63 Msamaria Mwema ........ 24
Somo la 64 Isaka na Visima Alivyochimba ........ 26
Somo la 65 Mwanamke Aliyeshiriki Chakula Chake ........ 28
**Nyimbo za Kutumia** ........ 30



Somo 53

# MARAFIKI WA PAULO

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Tunao marafiki kanisani.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Ninyi

1. Mkaribishe kila mtoto kwa kumwita kwa jina lake.

Nyimbo:
"Marafiki"
"Jumapili Yenye Furaha"
"Napenda Kanisa"

Tumia picha namba 53.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Matendo 18:1-3 na Warumi 16:3-4

Paulo alisafiri hadi sehemu nyingi sana. Alihubiri katika miji mingi. Wakati mmoja katika safari zake, alifanya urafiki na Akila pamoja na mkewe, Prisila. Walikuwa wakiishi katika mji wa Korintho.

Paulo alikuwa mhubiri, pia mshonaji mahema. Akila na Prisila nao walikuwa pia washonaji mahema. Paulo aliishi nyumbani kwao na wote walishirikiana kushona mahema.

Kila wiki, Paulo alienda kuabudu katika sinagogi. Akawahubiria injili ya Kristo. Akila na Prisila walikuwa wakienda naye kila wakati. Nao pia walikuwa wamemwamini Yesu Kristo. Kwa hivyo walimsaidia Paulo kueneza injili ya Yesu.

Paulo alienda Efeso pamoja na marafiki hao, baada ya kutoka Korintho. Kanisa walilolianzisha hapo, lilikutana nyumbani kwao. Walikuwa marafiki wema sana kwa Paulo na walimsaidia sana katika kueneza habari za Yesu.

Unapo waambia watoto hadithi hii ya Paulo na marafiki zake aliowapata kanisani, jaribu kuwasaidia waelewe kwamba wale watu wazima wawapatao kanisani ni rafiki zao.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto kwa kumwita kwa jina lake. Pengine waweza kupata watoto wapya darasani mwako. Wakaribishe kwa wema ili wajisikie kuwa huru.
2. Wimbo: "Napenda Kanisa"
3. Sadaka: Mwambie mtoto mmoja achukue chombo cha sadaka. Wengine watapaswa kwenda mbele na kuweka sadaka zao humo chomboni.
4. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka hiyo.
5. Rekodi: Andika kila jina katika kitabu. Sasa ita majina hayo na uweke alama hii (✓) kwa wale waliohudhuria.
6. Mchezo: Waambie watoto wakae katika mviringo, na wewe mwalimu, ukae ndani ya mviringo huo. Rusha nyoya la kuku au ndege juu, angani. Halafu sema,



dada, nyanya au babu, na kadhalika.

7. Sema, "Hadithi yetu ya leo inahusu jamaa moja iliyoshiriki chakula chao na mhubiri." **Fungua Biblia yako katika 1 Wafalme 17** na usimulie hadithi ya:

## MWANAMKE ALIYESHIRIKI CHAKULA CHAKE

Mama mmoja na mwanawe waliishi katika nyumba moja ndogo sana. Mtoto huyo aliona jinsi mamake alivyopika mikate kila siku. Mamake alichukua unga na mafuta kidogo na kuvichanganya vyote pamoja. Alikanda unga huo hadi ulipokuwa kama mviringo.

Mama huyu anapika mkate huo akitumia mawe yaliyo na moto mwingi. Mtoto wake alifurahia sana mkate uliyopikwa jinsi hiyo.

Mwaka huu hapakuwa na mvua, kwa hivyo hapakuwa na mazao yo yote shambani. Watu walisikia njaa sana. Kijana huyu mdogo na mamake hawakuwa na chakula cha kutosha.

Mama yake alikuwa amebaki na unga kidogo tu pamoja na mafuta. Kwani angeweza kutengeneza mkate na kula mara moja tu. Hata hakujua angepataje unga na mafuta mengine. Wakati wangemaliza chakula walichonacho, nao pia wangekuwa na njaa.

Mama huyo alienda kuokota kuni za kupika. Alikuwa anataka kwenda kupika mkate wao wa mwisho. Alipokuwa njiani, alikutana na mhubiri, Eliya. Alikuwa amesafiri kwa muda mrefu sana. Kwa hivyo alikuwa amechoka, pia mwenye njaa na alikuwa na kiu sana.

"Tafadhali, unaweza kunisaidia na maji ya kunywa? Nimesafiri kwa muda mrefu sana na ninasikia kiu," akamwambia.

Mwanamke huyo alimletea maji. Baadaye Eliya alimwambia, "Tafadhali nipatie na mkate, pia."

"Oh, samahani sana," mwanamke akamjibu. "Nimebaki na unga kidogo tu pamoja na mafuta. Nami nataka nimpikie mkate mwanangu tu."

"Usiwe na wasi wasi," Eliya akamwambia. "Nifanyie mkate kidogo kwanza na uniletee, kisha ujifanyie wewe mwenyewe pamoja na mwanao. Kwani Mungu ameahidi kwamba kutakuwa na chakula cha kututosha sisi wote."

Alipika mkate huo na akampatia Eliya. Alibaki na unga mwingine. Unga huu ulitosha kupika mkate wa mwanawe pamoja na yeye mwenyewe.

Aliweza kupika mkate kila siku. Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha. Vyote vilikuwa na chakula cha kutosha. Mungu aliwapatia chakula hicho kwa sababu walishiriki na mwenzao kile kidogo walichokuwa nacho.

8. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya chakula alichompatia mwanamke yule pamoja na mwanawe.
9. Wimbo: "Najua Mungu Ananitunza"
10. Chagua watoto watatu. Mmoja awe mama, mwengine awe mwanawe na mwingine awe mhubiri Eliya. Waambie waige mchezo wa hadithi hii. Rudia mchezo huo pamoja na watoto wengine watatu.
11. Fungua Biblia yako katika Yohana 15:17 na usome kifungu hicho, "Mpate kupendana." Waambie watoto kushikana mikono katika mviringo. Sasa semeni kifungu hicho pamoja.
12. Wimbo: "Jumapili Yenye Furaha"
13. Waonyeshe picha namba 65. Waonyeshe ni yupi Eliya, mhubiri. Uliza, "Je, mwanamke huyu ameshika nini mkononi mwake? Je, mnafikiri kuna nini katika mtungi ule?" Ongea kuhusu vitu ambavyo wanaweza kushiriki na wenzao.



Somo la 65

# MWANANKE ALIYESHIRIKI CHAKULA CHAKE

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Tunaweza kushiriki vitu tulivyonavyo na wenzetu.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mpate kupendana" (Yohana 15:17)

Nyimbo:
"Najua Mungu Ananitunza"
"Njia ya Furaha"
"Jumapili Yenye Furaha"

Tumia picha namba 65.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 1 Wafalme 17:8-16

Watu wa Israeli walikuwa wameanza kuabudu sanamu. Mungu aliwaadhibu kwa kuwaletea ukame nchini mwao. Kukawa hakuna chakula cha kutosha watu wote.

Eliya alikuwa nabii wa Mungu. Mungu alinena naye na kumwambia aende katika mji wa Serepta. Akamwambia, "Nenda kwa kuwa mjane mmoja atakutunza."

Eliya alikutana na mwanamke huyo karibu na lango kuu la mji. Akamletea maji ya kunywa. Alikuwa amebakiwa na unga kidogo tu pamoja na mafuta ya kuwatosha na chakula kingine cho chote. Soma tena vifungu hivyo. Twasoma katika kifungu cha 15 kwamba, "Akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi."

Watoto watajifunza kwamba Mungu hufurahi tunaposhirikiana na wenzetu. Mungu anatuhitaji pia kushiriki na wahubiri wetu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika. Sema, "Nimefurahi kwa sababu ________ amefika leo."
2. Imbeni wimbo usemao, "Njia ya Furaha," watoto wanapoenda mbele na kutoa sadaka zao.
3. Omba na umshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka hiyo.
4. Jaribu kuwatambulisha wale waliohudhuria kila jumapili kwa muda wa miezi mitatu mfululizo. Ita kila jina na uweke alama katika kitabu chako.
5. Mchezo: Mpe kila mtoto mbegu tatu za maharagwe. Nawe pia uwe na maharagwe matatu. Sema, "Nitashiriki maharagwe niliyo nayo kwa kumpa________," (sema jina la mtoto mmoja). Mpe maharagwe mawili au matatu. Naye atampatia pia mwenzake maharagwe mengi jinsi apendavyo. Endelea vivyo hivyo hadi kila mmoja atakapompatia mwenzake sehemu yake ya maharagwe.
6. Uliza, "Je, ulifurahi ulipomgawia mwenzako maharagwe yako? Jambo hili lilimpendeza Mungu. Sisi hushiriki katika jamaa zetu. Je, jamaa yako ni nani?" Ngojea watoto wajibu. Wengi wao watasema baba na mama, kaka,



"Unyoya huu unaanguka chini. ________, (sema jina la mtoto mmoja) njoo ushike unyoya huu kabla haujaanguka chini."

Mtoto huyo anaweza pia kurusha juu nyoya hilo na kuita jina la rafiki yake. Rudia mchezo huu hadi watoto sita au wanane watakapoucheza.

7. Sema, "Sisi huwa na wakati mzuri tukiwa pamoja na rafiki zetu. Nimefurahi kwa sababu rafiki zangu wamefika kanisani leo."
8. Wimbo: "Marafiki"
9. **Fungua Biblia yako katika Matendo 18** na useme hivi, "Biblia inatuambia habari za rafiki wema." Simulia hadithi ya:

## MARAFIKI WA PAULO KANISANI

Paulo alitaka kuwaambia watu habari za Yesu. Kwa hivyo, aliondoka nyumbani kwake huko Athene na kwenda katika mji wa Korintho. Alianza kuongea na watu akiwaambia kwamba Mungu anawapenda. Baadhi ya watu hao walimsikiliza kwa makini sana.

Alikutana na watu wawili, yaani mume na mke. Walisikiliza kwa makini kila neno alilosema Paulo. Wakapendezwa naye sana. Yule mume alikuwa akiitwa Akila, na mkewe, Prisila. Wao walimpenda Yesu sana na walitaka wampendeze Mungu kwa kila jambo. Hata walifurahia sana kuja kwa Paulo mjini kwao.

Paulo hakuwa na nyumba huko Korintho. Kwa hivyo alikuwa akitafuta mahali pa kuishi. Akaenda kuwatembelea rafiki hao wake. Waliongea kuhusu mambo mengi. Akila akamwuliza Paulo, "Je, utakuja kuishi pamoja nasi? Tuna chumba ambacho tunataka wewe uishi humo."

Paulo alitabasamu tu alipoambiwa hivyo. Alikuwa mwenye furaha sana. Akawaambia, "Mmekuwa wema sana kwangu. Nami nitafurahi sana nikiishi nyumbani kwenu."

Paulo alienda kuishi huko. Akaona jinsi Akila na Prisila walivyofanya kazi. Walikuwa wakishona mahema na kuyauza. Nao walifanya kazi kwa bidii sana. Walikata kitambaa hicho kwa makasi na kuanza kushona hema.

"Je naweza kuwasaidia?" Paulo akawauliza. "Mimi najua kushona mahema. Kwani, baba yangu alikuwa mshona mahema."

Akila na Prisila walifurahi sana kupata msaidizi. Paulo alikuwa mshonaji mzuri sana. Kwa hivyo, walishona mahema mengi sana na kuuza, wakati walipos aidiwa na Paulo.

Paulo aliishi Korintho kwa muda mrefu. Aliwaambia watu wengi sana habari za Yesu Kristo. Pia, alishukuru kwa kupata marafiki hao wapya.

Paulo alienda kanisani na kuwaambia watu habari za Yesu. Akila na Prisila walienda pamoja naye. Wote walishirikiana kuwaambia watu habari za Yesu.

Mwishowe, Paulo aliondoka Korintho na kwenda katika mji mwingine ili awaambie watu habari za Yesu. Akila na Prisila nao waliandamana naye hadi huko. Walikuwa tayari kumsaidia Paulo kwa jambo lo lote.

10. Fungua Biblia yako katika Yohana 15:14. Soma kifungu hicho, "Ninyi mmekuwa rafiki zangu." Waambie watoto wasimame na kushikana mikono wakiwa katika mviringo. Waambie sasa waseme kifungu hicho pamoja.
11. Wimbo: "Jumapili Yenye Furaha"
12. Waonyeshe picha namba 53. Mshukuru Mungu kwa ajili ya rafiki zako wajao kanisani.



Somo la 54

# SAMWELI NA ELI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Waalimu wa Shule ya Jumapili ni rafiki zetu.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Nawe mpende Bwana Mungu wako" (Marko 12:30).

Nyimbo:
"Njia ya Furaha"
"Marafiki"
"Naweza Kukua"

Tumia picha namba 54.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 1 Samweli 1:24-28; 2:11, 18; 3:1-10, 19

Eli alikuwa kuhani (Mchungaji) katika kanisa la Shilo. Aliwasaidia watu waliofika kwa Ibada.

Hana alifika kanisani kumwomba Mungu amjalie kupata mtoto. Alimwahidi Mungu kwamba angempa mtoto huyo amtumikie. Mtoto huyo alipokuwa mkubwa, Hana alitimiza ahadi yake.

Alimchukua mtoto huyo na kumpelekea Eli. Mchungaji huyu mzee sana alitakiwa kumfundisha mtoto huyo kazi ya kanisa.

Samweli aliishi na Eli. Alisaidia kwa kazi ya kanisa, na akawa anafungua milango yake. Pia, alipangusa na kuwasha taa za kanisani. Alimsaidia sana Eli ambaye alikuwa akizidi kuzeeka na kuwa kipofu.

Eli alimfundisha mtoto huyu habari za Mungu. Alimfundisha pia, jinsi ya kumtumikia na kumpendeza Mungu.

Kusudi la somo hili ni kuwafundisha watoto kwamba waalimu wao, pamoja na mchungaji, wanawapenda. Pia, tunataka kuwafundisha watoto njia tofauti za kumtumikia Mungu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1: Mkaribishe kila mtoto kwa kumwita kwa jina lake.
2. Waambie watoto kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka mara tu waingiapo darasani.
3. Mwambie kila mtoto asimame unapoita jina lake. Weka alama katika kitabu chako cha rekodi.
4. Wimbo: "Njia ya Furaha"
5. Mchezo: Waambie watoto hao kusimama wawili wawili. Ongea kuhusu marafiki. Sasa, mwulize kila mtoto kusema jina la rafiki yake aliyesimama naye.
6. Wimbo: "Marafiki"
7. Sema, "Hadithi yetu leo, inahusu mwalimu mmoja aliyemsaidia mtoto mdogo kujifunza habari za Mungu." **Fungua Biblia yako**



Baada ya kurudi darasani, utawagawa watoto hao katika makundi matatu. Lipe kila kundi matano au manane. Watatakiwa kuyaweka pamoja ili kutengeneza mfano wa kisima.

6. Sema, "Hadithi yetu ya leo yahusu mtu ambaye alijenga visima vitatu." **Fungua Biblia yako katika Mwanzo 26** na usimulie hadithi ya:

## ISAKA NA VISIMA ALIVYOCHIMBA

Isaka alikuwa na kondoo pamoja na ng'ombe wengi sana. Mifugo hao walihitaji maji na nyasi, ambavyo ni chakula chao. Isaka aliwapeleka ng'ombe wake katika bonde la majani mabichi. Hii ilikuwa sehemu ambayo babake aliishi zamani. Naye alivipata vile visima vilivyochimbwa na babake.

Visima hivi vilikuwa vimejaa uchafu kwa hivyo hakuweza kupata maji humo ya kuwanywesha mifugo wake. Isaka akawaambia watumishi wake, "Ondoeni takataka hiyo na mchimbe tena visima hivyo. Hasa, mifugo wetu wanahitaji maji ya kunywa."

Watumishi hao waliondoa takataka hiyo na wakapata maji masafi ya kuwapa mifugo wao.

Watu wengine waliwajia watumishi hao. Wakawaambia, "Maji haya ni yetu, nanyi hamwezi kuishi hapa." Watumishi hao walimwambia Isaka yale waliyoambiwa, naye akawaambia, "Basi, tutaondoka mahali hapa kwa sababu hatutaki ugomvi."

Isaka aliwapeleka jamaa yake, watumishi na mifugo wake mahali pengine. Watumishi wake walichimba tena kisima mahali hapo. Watu wengine waliwajia tena watumishi wa Isaka na kuwaambia, "Maji haya ni yetu. Na ni lazima mtuachie."

Isaka alipata habari ya kitendo hicho, "Basi tutaondoka mahali hapa, kwani hatutaki ugomvi," akawaambia.

Ilimbidi Isaka awahamishe tena jamaa yake, watumishi na mifugo yake hadi sehemu nyingine. Wakati huu alimwomba Mungu aweze kumsaidia.

Usiku huo huo aliota ndoto. Mungu alisema naye. Akamwambia, "Umefanya jambo lililo jema. Nami nitakutunza na kukulinda."

Baadaye, watumishi wa Isaka walichimba kisima kingine. Walienda kwa haraka na kumwambia Isaka, "Tumepata maji yaliyo masafi sana."

Isaka akawajibu, "Hii ni siku jema. Nimefurahi kwa sababu tumempendeza Mungu sana.

7. Sema, "Mungu hufurahi tunapowasamehe wenzetu. Anatutaka tuwe wema. Leo tunacho kifungu muhimu sana ambacho tutajifunza." Soma Waefeso 4:32, "Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi." Waulize watoto kutaja njia ambazo wanaweza kuonyesha wema wao.
8. Wimbo: "Marafiki"
9. Waambie watoto kusimama katika mviringo. Mgonge mtoto mmoja unapotembea katika mviringo huo; mwambie, "samahani." Baadaye tena, kanyanga vidole vya mguu vya mtoto mwingine; Mwambie, "samahani sana." Mwishowe wasukume kando watoto wawili ili upite katikati yao. Waambie pia "samahani sana."

   Uliza, "Je, niliwaambia nini?" "Ndiyo nilisema 'Samahani sana.' Nataka mnisamehe kwa sababu nimewakosea."
10. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema"
11. Mwombe Mungu amsaidie kila mmoja wenu kuwa mwema kwa wenzake.



Somo la 64

# ISAKA NA VISIMA ALIVYOCHIMBA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Inatupasa kuwasamehe wengine.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi" (Waefeso 4:32).

Nyimbo:
"Njia ya Furaha"
"Marafiki"
"Nisaidie Kuwa Mwema"

Tumia picha namba 64.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 26:17-33

Isaka alikuwa mmoja kati ya watu waliompendeza Mungu. Alikuwa mtoto wa Abrahamu na Sarah. Yeye pia aliambiwa ahadi ile ile Mungu alimwambia Ibrahimu, babake: "Nitakuzidishia uzao wako kama nyota angani. Na nitawapa nchi hii yote, nao watakuwa baraka kwa mataifa mengine yote duniani."

Kulikuwa na ukame katika nchi yao. Naye Mungu akamwongoza Isaka hadi mahali paitwapo Gerari. Isaka alipanda na kufanikiwa na mazao mengi sana. Pia, alikuwa na ng'ombe wengi pamoja na kondoo. Huyo basi, alikuwa na utajiri mwingi sana. Mfalme wa nchi hiyo alimwambia Isaka aondoke kwake na kwenda kuishi mahali pengine.

Isaka alianza safari. Alifuata njia zile zile baba yake Ibrahimu alifuata zamani zake. Vile visima ambavyo Ibrahimu alikuwa amevichimba zamani, sasa vilikuwa vimejazwa na takataka. Kwa hivyo, ilimbidi Isaka na watu wake kuchimba visima vingine. Wachungaji wa sehemu hiyo walipoona visima hivyo, walianza kusema kwamba ni vyao. Hapo, ugomvi ulizuka baina ya wachungaji wa Isaka na watu hao.

Isaka na watu wake walienda mahali hapo na kwenda kuchimba kisima kingine tena. Hata hicho nacho, kilisemekana kuwa cha wachungaji wa sehemu ile.

Isaka na watu wake waliondoka tena mahali pale na kwenda kuishi sehemu ya mbali sana. Wakati huu, aliweza kutumia na kumiliki visima vyote alivyochimba.

Mungu alipendezwa sana na Isaka. Yeye hakutaka ugomvi, bali alikuwa na moyo wa kuwasamehe wale waliomkosea.

Somo hili litawasaidia watoto kujifunza kuwa na moyo wa kuwasamehe wale wanaowakosea.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto afikapo.
2. Imbeni wimbo usemao, "Njia ya Furaha," watoto waendeleapo kutoa sadaka zao.
3. Mshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka hiyo.
4. Rekodi: Ita kila jina na uweke alama katika kitabu chako kando ya wale waliohudhuria.
5. Wapeleke watoto nje kwenda kuokota mawe madogo madogo. Watahitajika kuwa na mawe 25.



**katika 1 Samweli na usimulie hadithi ya:**

## SAMWELI NA ELI

Samweli alipenda sana kwenda kanisani. Pia, alimpenda sana mchungaji Eli. Eli alikuwa akizeeka, kwa hivyo alihitaji mtu wa kumsaidia. Samweli aliamua kwenda kuishi na Eli na kuwa msaidizi wake. Samweli alifunga milango ya kanisa kila jioni na kuifungua tena kila asubuhi. Watu wengi waliweza kufika na kuomba pamoja.

Samweli vile vile, alizitunza taa za kanisani. Aliziwasha kila mara na kuzipangusa. Pengine alifagia kanisa hilo na kupangusa mavumbi kutoka vitini.

Samweli alifanya kile ambacho Eli alimwambia. Alisikiliza kwa makini, wakati Eli aliposoma Biblia ya kuviringisha. Hata alisikiliza pia alipoambiwa habari za Mungu na Eli.

Siku moja usiku, Samweli alikuwa akipumzika kitandani mwake. Akasikia mtu akimwita, "Samweli, Samweli."

Aliamka mara moja na kwenda chumbani mwa Eli. Akamwambia, "Mimi hapa." Eli naye akamjibu, "Sikukuita. Nenda ukalale." Samweli alilala tena. Akasikia sauti ikimwita, "Samweli, Samweli."

Samweli alienda tena kwa Eli. Lakini Eli akamwambia, "Sikukuita, mwanangu. Nenda ukalale."

Samweli alienda tena kitandani na kulala. Kwa mara nyingine, alisikia sauti hiyo hiyo ikimwita. Aliamka tena na kumwendea Eli.


Wakati huu Eli alitambua kwamba Mungu ndiye aliyekuwa akimwita Samweli. Akamwambia, "Nenda ukalale. Lakini utakapoitwa tena sema hivi, 'Nena, Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikia.' "

Samweli alifanya jinsi Eli alivyomwambia. Alipoisikia tena sauti hiyo, alisema, "Nena Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikia."

Mungu alimwambia Samweli kwamba anamtaka afanye kazi maalum. Mungu alimtaka Samweli awe mhubiri. Alimtaka naye awafundishe wengine jinsi Eli alivyokuwa akifanya.

Samweli alifanya kazi kanisani kwa bidii sana kila siku. Alijifunza kila siku pia, kutoka kwa mwalimu wake, Eli.

8. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya waalimu wajao kanisani.
9. Waambie watoto kwamba, "Samweli alienda kuishi kanisani alipokuwa mdogo sana. Mwishowe alikuwa mkubwa. Hata akajifunza kutoka kwa mwalimu wake, Eli. Sasa imbeni, "Naweza Kukua."
10. Sema, "Jambo mojawapo ambalo Samweli alijifunza ni kumpenda Mungu." Fungua Biblia katika Marko 12:30 na usome kifungu hicho, "Nawe mpende Bwana Mungu wako." Waambie watoto kurudia kifungu hicho hadi watakapokisema bila kusaidiwa.
11. Waonyeshe picha namba 54. Ongea nao kuhusu Samweli, Hana na Eli. Pengine wanaweza kutaka kuiga mchezo wa mambo yale ambayo Samweli aliyafanya hekaluni.



Somo 55

# UJENZI WA KANISA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Marafiki hufanya kazi pamoja kanisani.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Fanya kazi kwa mikono yenu wenyewe" (1 Wathesalonike 4:11).

Nyimbo:
"Msaidizi Nakuwa"
"Napenda Kanisa"
"Marafiki"

Tumia picha namba 55.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Kutoka 35, 36

Musa alikuwa kiongozi wa watu. Aliwasaidia katika safari yao ya kutoka Misri kwenda "Nchi ya Ahadi."

Mungu alikuwa na mpango kwa watu wake. Walitakiwa kujenga hema kuliita "Nyumba Ya Mungu." Watu wote wangekutanika humo na kuabudu.

Watu wote waliishi katika mahema, kwa sababu hawakuwa wakiishi mahali pamoja. Nyumba ya Mungu nayo ilijengwa kwa hema. Wangeweza kuibomoa kwa urahisi na kuipeleka mahali pengine waendapo.

Walipomaliza ujenzi wa kanisa hilo, walilitoa hasa kwa utukufu wa Mungu. Kanisa hilo lilifunikwa na wingu na likajazwa na utukufu wa Bwana.

Unapowafundisha watoto, wasaidie wafahamu kwamba kila mmoja alisaidia kwa ujenzi wa kanisa hilo. Mungu alitarajia kwamba kila mmoja, yaani mama, baba na watoto kufanya kazi pamoja na kujenga mahali pa kufanyia ibada yao.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto anapofika.
2. Watoto wanatakiwa kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka mara tu wafikapo.
3. Ita kila jina. Mwambie mtoto huyo kusimama wima kama mti. (Atasimama na kuinua mikono yake juu). Weka alama hii (✓) kando ya jina la yule aliyehudhuria.
4. Wimbo: "Napenda Kanisa"
5. Uliza, "Je, tungetumia sadaka zetu za leo kwa kununulia kanisa letu nini?" Ngojea watoto wataje baadhi ya vitu wafikiriavyo. Kama wanahitaji msaada wako, basi waweza kusema, vitabu vya nyimbo, Biblia, kalamu, viti na kadhalika.
6. Wimbo: "Marafiki"
7. Fungua Biblia yako katika 1 Wathesalonike 4:11 na usome kifungu hicho, "Fanya kazi kwa mikono yenu wenyewe." Waambie wasichana waseme kifungu hicho peke yao kwanza, halafu tena wavulana wakiseme peke yao.



wingu." Kaa chini na uwe kimya kabisa.

6. **Fungua Biblia yako katika Luka 10** na usimulie hadithi ya:

**MSAMARIA MWEMA**

Siku moja palikuwa na mtu aliyekuwa akitoka Yerusalemu akienda Yeriko. Alitokewa na wanyang'anyi bila kutarajia. Wakamnyang'anya kila kitu alichokuwa nacho. Baadaye walimpiga na kumwacha amelala barabarani karibu ya kufa.

Mjeruhiwa huyo hakuweza kutembea. Akasikia hatua za mtu atembeaye. Lakini hakusimama ili amsaidie bali alienda zake tu. Alimsikia mtu huyo akitembea kwa haraka akienda zake.

Muda si muda, mjeruhiwa huyo alisikia mtu akitembea. Mtu mwingine alikuwa akija sehemu hiyo. Akawaza moyoni, "Mtu huyu ajaye atanisaidia." Lakini msafiri huyo alimwangalia tu na kuendelea na safari yake.

Mjeruhiwa huyo alikuwa ameumizwa sana. Alihitaji mtu wa kumsaidia. Baada ya muda, alisikia tena hatua za mtu atembeaye. Hakuwa mtu akitembea, bali alikuwa punda wa mtu fulani. Mjeruhiwa huyo alisikia mtu akimwambia punda wake asimame. Alipoangalia juu alimwona mtu akishuka kutoka kwa punda wake. Mtu huyo alikuwa ametoka Samaria.

Mtu huyo mwema alimwendea mjeruhiwa huyo. Akamwambia, "Nitakusaidia."


Alimweka dawa katika majeraha yake, halafu akavifunga vidonda hivyo. Alimbeba na kumweka juu ya punda wake, nao wakaanza safari.

Walipofika katika nyumba ya wageni, walisimama na mtu huyo akamsaidia mjeruhiwa wake kuingia ndani. Akamnunulia chakula na kumtafutia mahali pa kupumzikia.

Mjeruhiwa huyo alijisikia vizuri sana. Alikuwa amepata rafiki wa kumsaidia.

Siku iliyofuata, mtu huyo mwema aliendelea na safari yake. Alimwachia mwenye nyumba pesa za kulipia chakula cha mjeruhiwa huyo na za kumtunzia. Aliitwa Msamaria mwema kwa sababu alitenda mema.

7. Uliza, "Je, mnaweza kuniambia mambo yote mema ambayo mtu huyo alifanya?" Ngojea watoto wajibu. Sema, "Yesu anatutaka sisi pia kuwa wema."
8. Waonyeshe picha namba 63. Sema, "Je, mtoto huyu anafanya nini?" Je, anatenda mema?" Taja njia tofauti za kuwa wema kwa baba, mama au wageni.
9. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema"
10. Watoto watafurahi sana wakiiga mchezo wa "Msamaria Mwema." Usiwakubalie wale wachukuao sehemu ya wanyang'anyi kutenda mabaya zaidi.
11. Sema, "Biblia inatuambia kwamba inatupasa sisi kuwa wasaidizi." Soma Isaya 41:6, "Wakasaidiana, kila mtu na mwenzake."
12. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya wale watusaidiao.



Somo la 63

# MSAMARIA MWEMA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Twaweza kuwasaidia wenzetu.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Wakasaidiana, kila mtu na mwenzake" (Isaya 41:6).

Nyimbo:
"Njia ya Furaha"
"Nisaidie Kuwa Mwema"
"Msaidizi Nakuwa"

Tumia picha namba 63.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Luka 10:25-37

Mwana-sheria mmoja alimwuliza Yesu swali. Alitaka kumjaribu Yesu kwa kumwuliza swali hilo. Lakini Yesu alimjibu kwa kumwuliza swali hili, "Imeandikwa nini katika Torati?"

Soma jibu la mwana-sheria huyo katika kifungu cha 27. Yesu alikubaliana na jibu hilo lake. "Fanya hivi nawe utaishi," akamwambia.

Mwana-sheria huyo alimwuliza tena swali lingine. Akamwambia, "Na jirani yangu ni nani?"

Kulingana na Wayahudi, jirani yake alikuwa Myahudi mwenzake. Pia, kwa Wasamaria, alikuwa ni Msamaria mwenzake. Lakini kwa Yesu, jirani alikuwa ni kila mtu. Baadaye, alisimulia hadithi ya kuonyesha jirani ni nani.

Soma tena Luka 10:30-37. Utawasimulia watoto hadithi hii. Mhubiri na kiongozi wa kanisa walipita bila kujali mtu huyo aliyejeruhiwa. Hawakumsaidia. Msamaria tu ndiye aliyemsaidia mjeruhiwa yule. Kwa hivyo, yeye ndiye aliyekuwa jirani.

Unatakiwa kuwafundisha watoto kuwasaidia wenzao. Twajua kwamba Mungu anawapenda watu wote. Anatutaka sisi nasi kuonyesha upendo huu kwa wenzetu. Njia moja ya kuonyesha upendo ni kwa kutenda mema na kumsaidia kila mmoja.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto.
2. Pitisha chombo cha kuweka sadaka kwa kila mtoto. Mshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka hiyo.
3. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa"
4. Mwambie kila mtoto asimame unapoita jina lake. Atatakiwa kusimama vivyo hivyo hadi utakapoita watoto wengine wote.
5. Mchezo: Simameni katika mviringo. Sema, "Sasa tutakuwa wadogo sana kama panya." Mtatakiwa kuchuchumaa. Sasa sema, "Wakati huu, tutakuwa warefu kama nyumba." Simameni na muinue mikono yenu juu. "Sasa tutakuwa wapana kama mlango mkubwa." Simameni mmepanua miguu na mikono yenu. "Sasa nimetulia kama



Kirudie hadi watakapokishika sawasawa.

8. Sema, "Hadithi yetu ya leo inahusu watu ambao walifanya kazi pamoja na rafiki zao. Walilijenga kanisa la Mungu kwa kushirikiana." **Fungua Biblia yako katika kitabu cha Kutoka 35,** na usimulie hadithi ya:

## UJENZI WA KANISA

Watu wa Mungu walikuwa wamesafiri kwa muda mrefu sana. Walikuwa wakienda katika nchi geni. Wangetakiwa sasa kujenga nyumba zao. Mungu alikuwa amewatunza na kuwalinda katika safari hiyo yao. Aliwapatia chakula waliposikia njaa. Akawapa maji walipokuwa na kiu.

Watu hao walienda safari ndefu sana kila siku. Wakati wa usiku walijenga nyumba zao za mahema na wakalala humo. Ilipofika asubuhi, walibomoa mahema hayo na kuendelea na safari yao.


Watu hao walijisikia wachovu sana. Siku moja, Mungu alisema na kiongozi wao, Musa. Akamwambia, "Waambie watu hao wanijengee nyumba. Itakuwa hema. Nayo nitaishi pamoja nao." Mungu alitaka watu wao wajue kwamba yu karibu nao. Wangeweza kuiona mara kwa mara, nyumba hiyo ya Mungu.

Mungu alimtaka kila mtu kutoa kitu cho chote kwa ajili ya nyumba yake. Akamwambia Musa, "Waambie watu wote ambao mioyo yao imewapa kupenda wanitolee sadaka. Mwache mtu ye yote mwenye moyo wa kupenda ayalete matoleo."

Watu wa Mungu walifurahi sana. Walikuwa na moyo wa kumjengea Mungu nyumba. Walifurahi sana walipoleta matoleo yao katika nyumba ya Mungu. Baadhi yao walimtolea dhahabu na fedha. Wanawake wengine nao walishona pazia na kumtolea Mungu. Vyote vililetwa ndani ya nyumba ya Mungu. Baadhi yao hawakufanikiwa na kitu cha kumtolea Mungu. Lakini walisaidia katika ujenzi wa kanisa hilo. Wote walifanya kazi pamoja ili kujenga na kupamba kanisa hilo.

Hatimaye walimaliza ujenzi wa kanisa hilo. Walilijenga jinsi Mungu alivyowaambia. Watu walipoiona nyumba ya Mungu walijua kwamba yu pamoja nao.

9. Tengenezeni kanisa la hema. Jaza mchanga katika kisanduku, au mkebe, au chombo kingine kidogo. Tumia vijiti kutengeneza hatua zenye pande nne mraba: Vijiti hivyo vitatakiwa kuwa na urefu wa sentimita 20-25. Weka kitambaa, au shuka ndogo juu ya vijiti hivyo.
10. Wimbo: "Napenda Kanisa"
11. Waonyeshe picha namba 55. Waambie watoto kwamba jengo hilo lililozungukwa na ukuta ndilo kanisa lenyewe. Uliza, "Je, linafanana na mfano huu tuliotengeneza?"
12. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya kanisa lako na sadaka mlizotoa siku ya leo.
13. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa"



Somo 56

## MSAADA KWA MARAFIKI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Marafiki wa kanisani hushiriki vitu vyao na wenzao.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Jifunzeni kutenda mema" (Isaya 1:17).

Nyimbo:
"Marafiki"
"Napenda Kanisa"
"Leo Tunafuraha"

Tumia picha namba 56.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Matendo 11:27-30, 1 Wakorintho 16:2, 2 Wakorintho 8:1-15

Agabusi alikuwa nabii katika Agano Jipya. Aliwaambia watu kwamba kutakuwa na njaa katika nchi ya Israeli. Hata hakutakuwa na chakula cha kutosha kwa kila mtu.

Wakristo wa Antiokia walitaka sana kuwasaidia watu wa kanisa la Yerusalemu. Kila mmoja alitoa zawadi yake ili kuwasaidia. Paulo na Barnaba ndio waliopeleka chakula hicho na pesa, huko Yerusalemu.

Soma 1 Wakorintho 16:2. Paulo anatufundisha kwamba tunatakiwa kutoa sadaka zetu kila Jumapili. Tunapaswa kumtolea Mungu kama zawadi.

Soma 2 Wakorintho 8:1-15. Paulo alitembelea makanisa ya Makedonia. Akawaeleza kuhusu waamini wa Yerusalemu. Wengi wao walikuwa maskini. Walinyang'anywa mashamba na mali zao walipomkubali Kristo na kuwa Wakristo. Paulo aliwaambia wakristo wa Makedonia wawasaidie Wakristo wenzao walioko Yerusalemu. Hata ingawa nao pia walikuwa maskini, walitaka sana kuwasaidia wenzao. Waliwapelekea Wakristo wa Yerusalemu zawadi, misaada na barua za kuwatia moyo kwa sababu walimpenda Mungu sana.

Mungu anatarajia kila mmoja (hata watoto) kumtolea sadaka. Watoto watajifunza kwamba hii ni njia mojawapo ya kuabudu. Sadaka zetu ni njia mojawapo ya kushiriki vitu tulivyonavyo na wenzetu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Msalimie kila mtoto anapofika.
2. Wimbo: Imbeni wimbo usemao, "Marafiki" wanapoendelea kufika.
3. Waambie watoto wakae katika mviringo. Wape chombo cha sadaka. Kila mmoja atoe sadaka yake.
4. Maombi: Omba hivi, "Asante sana, Mungu, kwa pesa tulizonazo ambazo twaweza kushiriki na wenzetu. Amina."



3. Wimbo: "Marafiki"
4. Mchezo: Simama mbele ya darasa na useme. "Nitacheza peke yangu, nitacheza peke yangu. Je, nani anataka kucheza nami? La, la, la, la." Baada ya kuuliza swali hilo, mchague mtoto mmoja na mshikane mikono. Imbeni naye hivi, "Twacheza peke yetu. Nani atakaye kucheza pamoja nasi? La, la, la, la." Endelea na mchezo huu hadi watoto wote watakaposhikana mikono na kuimba pamoja.
5. Sema, "Je, mmewahi kutembelewa na mgeni wiki hii?" Waambie waeleze kuhusu yule aliyewatembelea na kule alikotoka. "Je, mama yako alifanya nini wakati wa kumkaribisha?" Zungumzia kuhusu njia mbali mbali za kuwasaidia wageni.
6. **Fungua Biblia yako katika Yohana 4** na usimulie hadithi ya:

### YESU AKUTANA NA MWANAMKE KISIMANI

Kulikuwa na joto sana huko Samaria. Lakini mwanamke mmoja alichukua mtungi wake wa maji na akajitwika kichwani. Alienda haraka hadi kisimani.

Alipofika kisimani, alimkuta mtu akiwa amekaa hapo. Alikuwa akipumzika tu. Hakumtambua kwa sababu hakuwa Msamaria. Bali alikuwa Myahudi.

Alianza kuchota maji yake haraka haraka. "Tafadhali nipe maji ninywe," mtu huyo akamwambia. Mtu huyo alikuwa Yesu.

Mwanamke huyo alishangaa sana alipoombwa maji. "Wewe ni Myahudi nami ni Msamaria. Je, mbona waniomba maji?" akamwambia.

Yesu aliongea na mwanamke huyo kwa muda mrefu sana. Alimweleza mambo mengi kuhusu Mungu.

"Mungu anakupenda," akamwambia.

"Najua kwamba Mungu atamtuma Mwanawe hivi karibuni," mwanamke huyo akamwambia.

"Mungu ameshamtuma Mwanawe," Yesu akamjibu. "Mimi ndiye Yesu, Mwana wa Mungu."

"Wewe ndiye kweli Mwana wa Mungu?" Mwanamke huyo akamwuliza. "Ni lazima niwapashe rafiki zangu habari. Nataka kila mmoja amtambue Mwana wa Mungu."


Mwanamke huyo alirudi mbio hadi kijijini. Akamwambia kila mtu amfuate hadi kisimani.

"Njooni kisimani. Mwana wa Mungu yuko hapo. Njooni mmwone," akawaambia.

Marafiki wa mwanamke huyo walikusanyika karibu na Yesu. Wakisikiliza kwa makini yale aliyowaambia. Nao walimwuliza maswali mengi sana.

Yesu na wanafunzi wake walienda hadi kijijini mwao. Walikaa huko kwa muda wa siku mbili wakiwaambia watu kuhusu upendo wa Mungu.

7. Waonyeshe picha namba 62. Uliza, "Je, mnaona nini katika picha hii? Ninyi huchota maji wapi?" Kama maji yao hayachotwi katika mifereji iliyoko ndani ya nyumba yao, basi waweza kuwaelezea jinsi ya kupata maji. Je, nani hubeba maji hayo? Wao huona akina nani waendapo kuchota maji?
8. Nyimbo: "Yesu Anipenda"
"Nisaidie Kuwa Mwema"
9. Fungua Biblia yako katika 1 Yohana 4:10 na usome kifungu hicho, "Mungu...alitupenda sisi, akamtuma mwanawe." Rudieni pamoja kifungu hiki.
10. Maombi: Mshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu.



Somo 62

## YESU AKUTANA NA MWANAMKE KISIMANI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu anampenda kila mmoja.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu... alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe" (1 Yohana 4:10).

Nyimbo:
"Yesu Anipenda"
"Marafiki"
"Nisaidie Kuwa Mwema"

Tumia picha namba 62.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Yohana 4:1-42

Vifungu hivi vyahusu kukutana kwa Yesu na mwanamke Msamaria. Wasamaria walikuwa mchanganyiko wa kabila la watu waliozaliwa na wanawake wa kiyahudi walioolewa na watu wa makabila mengine. Kwa hivyo, Wayahudi na Wasamaria walichukiana sana. Hata hawakuweza kusimama na kuongea pamoja.

Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakitoka Yerusalemu wakienda Galilaya. Njia ya kuwafikisha huko haraka ilipitia Samaria. Yesu alikuwa amechoka sana. Kwa hivyo, yeye alikaa kisimani wakati wanafunzi wake walipokwenda mjini kununua chakula. Hapa ndipo alipokutana na mwanamke huyu.

Yesu aliamua kuwa rafiki wa mwanamke huyu pamoja na Wasamaria wengine. Ona jinsi alivyoongea na mwanamke huyu kwa mara ya kwanza akimwambia hitaji lake. Alikuwa na kiu, na mwanamke huyu tu ndiye angempatia maji.

Baadaye, aliongea kuhusu mwanamke yule aliye na dhambi. Angeweza kumwonyesha jinsi ya kumwabudu Mungu kwa moyo safi. Yesu pamoja na wanafunzi wake walikaa katika kijiji hicho kwa muda wa siku mbili. Waliwasaidia watu wengi kumwamini Mungu.

Kumbuka kwamba unawafundisha watoto wadogo sana ambao hawajui dhambi ni nini. Soma tena maandiko ya somo hili. Yesu alikuwa mgeni tu. Alikuwa akipita katika kijiji hicho. Naye alikuwa amechoka sana na mwenye kiu. Mwanamke mmoja alikuwa mwema kwake na akampatia maji ya kunywa.

Naye Yesu, alimsaidia pia. Alikuwa mwema kwake hata ingawa yeye alikuwa mwanamke mwenye dhambi. Unaweza kuwasaidia watoto kuelewa kwamba wanaweza kuwa wema kwa wageni. Hii ni njia mojawapo ya kuonyesha upendo wa Mungu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto.
2. Waambie watoto watembee katika mviringo huku wakiweka sadaka zao katika chombo cha sadaka.



5. Wimbo: "Napenda Kanisa"
6. Uliza, "Kwa nini unapenda kuja kanisani?" Ngojea watoto wajibu. Sema, "Tukiwa kanisani, hujifunza jinsi ya kushiriki vitu vyetu na wenzetu. Je, sisi hushiriki nini?" Watoto wanaweza kusema vitabu, picha, sadaka na kadhalika.
7. Mwulize mtoto mmoja kufanya kitendo jinsi awezavyo kushirikiana na rafiki zake. Watoto wengine wanaweza kubahatisha kile kitendo au kitu afanyacho. Waweza kuwaambia watoto wawili au watatu kufanya hivyo. Kwa mfano, anaweza kusoma kitabu, kukaa kwa mkeka au kutoa zawadi.
8. Fungua Biblia yako katika kitabu cha Isaya 1:17 na usome kifungu hicho, "Jifunzeni kutenda mema." Sema kifungu hicho pamoja na watoto.
9. Sema, "Hadithi yetu ya Biblia inatuambia habari za Wakristo fulani walioshiriki mali zao na rafiki zao. Walifurahia sana kuwasaidia wenzao. Waliposhiriki mali zao, walikuwa wakitenda mema." **Fungua Biblia yako katika Matendo 11** na usimulie hadithi ya:

### MSAADA KWA MARAFIKI

Paulo na Barnaba walienda kuwatembelea washiriki wa kanisa la Antiokia. Waliwafundisha habari za Yesu. Wakawaambia jinsi Yesu alivyowasaidia watu wengine.

Watu walioishi Yerusalemu hawakuwa na chakula cha kutosha. Kwa sababu kulikuwa na njaa kuu nchini humo.

"Hapa Antiokia tuna chakula. Hatuna njaa." Mkristo mmoja akawaambia.

"Tumejifunza kwamba Yesu aliwasaidia watu wengine. Nasi twaweza kuwasaidia rafiki zetu," mtu mwingine akasema.

Kila mmoja alijisikia kuwa na mwito wa kusaidia. Walianza kupanga jambo la kufanya.

Mmoja wao akasema, "Kila mmoja wetu anaweza kutoa cho chote alichonacho kwa ajili ya rafiki zetu."

"Ndiyo. Baadhi yetu wanaweza kutoa pesa. Na wengine chakula. Sote tunaweza kushirikiana," mwingine akajibu.

Kila mmoja alitoa jinsi awezavyo. Waliokuwa na vitu vingi walitoa zaidi. Waliokuwa na mali kidogo, nao walitoa kulingana na uwezo wao. Walipoweka zawadi hizo pamoja, walipata kuwa wamekusanya mali nyingi sana.

Wakawaambia Paulo na Barnaba wawasaidie. Waliambiwa wawapelekee rafiki zao mali hiyo waliyoikusanya. Iliwafanya watu kuwa na furaha kwa kuwa waliweza kushiriki na wenzao. Walifurahi pia kwa sababu waliweza kuwasaidia rafiki zao.

10. Waonyeshe picha namba 56. Uliza, "Ni nani unayemwona katika picha hii? Je, wanafanya nini? Je, unafikiri mchungaji na mwanamke huyo Mkristo wamemletea mwanamke masikini chakula?"
11. Wimbo: "Leo Tunafuraha"
12. Mshukuru Mungu kwa sababu sote twaweza kushiriki mali zetu.



Somo la 57

## FILIPO ASHUHUDIA UPENDO WA MUNGU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu anampenda kila mmoja.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu ni upendo" (1 Yohana 4:8).

Nyimbo:
"Yesu Anipenda"
"Nampenda Yesu"
"Yesu Apenda Watoto Wote"
"Napenda Kanisa"

Tumia picha namba 57.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Matendo 8:25-40

Filipo alikuwa shemasi (mzee wa kanisa) katika kanisa la Yerusalemu. Alikuwa amechaguliwa ili awasaidie viongozi wa kanisa hilo. Katika Matendo 6:3, tunaambiwa kwamba alikuwa, "mwenye kujawa na Roho, na hekima."

Siku moja malaika alimwambia kwamba, "Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza" (Matendo 8:26). Filipo alitii ujumbe huo wa Mungu. Alimwona mtu akiwa ndani ya gari lake. Mtu huyo alikuwa akisoma Biblia ya kuviringisha.

Mtu huyu hakuwa Myahudi bali alikuwa akitoka Kushi (Ethiopia). Alikuwa amesafiri safari hiyo ndefu ili kwenda na kumwabudu Mungu hekaluni. Basi, alipokuwa akirudi nyumbani, alianza kusoma maandiko ya Kitabu cha nabii Isaya.

Roho wa Mungu alisema na Filipo. Akamwambia, "Nenda karibu na gari hilo." Alipoenda alimsikia mtu huyo akisoma maandiko. Naye akamwuliza, "Je, unaelewa hayo usomayo?"

Hatimaye, Filipo alimweleza maana ya maneno hayo. Soma Isaya 53. Filipo alimwambia habari za Yesu. Akamwelezea jinsi Yesu alivyokufa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Mtu huyo wa Kushi alimkubali Yesu kuwa Mwokozi wa maisha yake.

Filipo alikuwa Myahudi, na mtu huyo mwingine alikuwa mtu wa kushi. Mungu aliwapenda wote. Pia, Mungu anawapenda watu wote.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto anapofika. Imbeni, "Yesu Apenda Watoto Wote." Tumia jina la mtoto mmoja badala ya "watoto wote." Kwa mfano, "Yesu Anapenda 'Mariamu'." Imbeni tena mkitumia jina la mtoto mwingine.
2. Watoto wanaweza kufika na kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka.
3. Wimbo: "Napenda Kanisa"
4. Uliza, "Je, mlikujaje kanisani leo?" Waache watoto waige vile walivyokuja. Wakitembea kwa mguu, au wakiendesha baisikeli, au pengine walipanda gari. Baadaye waeleze njia zingine za kusafiria, kama: ndege, gari la



6. Sema, "Ni nani aliye na ndugu mchanga wa kiume?" Je, wewe husaidia kwa kumtunza mtoto huyo? Je, wewe husaidiaje?" Ngojea watoto waseme njia ambazo hutumia kwa kumtunza mtoto huyo.
7. Sema, "Leo nitawaambia hadithi ya mtoto mmoja aliyezaliwa katika jamaa iliyo na furaha. Alikuwa na mama, baba, ndugu na dada." **Fungua Biblia yako katika Kutoka 2** na usimulie hadithi ya:

**JAMAA YA MTOTO MUSA**

Mtoto Musa alikuwa mwenye afya nzuri. Kila mara alikuwa mwenye furaha. Alikuwa pia na ndugu na dada mkubwa kwake.

Jamaa yake, walimpenda sana. Lakini walitakiwa kuwa waangalifu. Walipaswa kumficha mtoto huyo ili awe salama, kwa sababu mfalme alikuwa ameamuru kwamba watoto wote wadogo wa kiume wauawe.

Miriamu, dada yake, alisaidia sana kwa kumtunza mtoto huyo. Siku moja mamake alimwambia, "Mtoto Musa ameanza kuwa mkubwa. Yeye hulia na kucheka kwa sauti kubwa sana. Ni lazima tutafute njia nyingine ya kumficha."

Mamake alianza kutengeneza kikapu cha kisafina. Alikitengeneza vizuri sana. Akakipaka lami ili maji yasiingie ndani.

"Miriamu, mfunge mtoto huyo katika blanketi, na unifetee," mamake akamwambia.

Walimweka Musa katika kisafina hicho na kumpeleka mtoni. Wakakiweka majini kando ya mto. Nacho kikaelea juu ya maji. Humo ndani, mtoto Musa alikuwa mkavu na pia salama.

"Ni lazima ukae hapa na kumlinda mtoto huyu," Miriamu akaambiwa na mamake.

Baada ya muda mfupi, Miriamu alimsikia mtu akija. Alipoangalia alimwona Binti ya mfalme akija. Alikuwa akija kuoga katika mto huo. Binti huyo alipokiona kisafina hicho, alisema, "Nileteeni kisafina hicho."

Alikifungua ndani na kumwona mtoto akiwa amelazwa humo. "Huyu ni mtoto wa Kiebrania, lakini namtaka awe wangu. Nataka nimtunze kama mtoto wangu," Binti huyo akasema.

Miriamu alikimbia hadi kwa Bintiye mfalme na akamwuliza, "Je, niende nikakwitie mlezi?"

Miriamu aliendа kwa haraka na akamwita mamake. Mwanamke yule alimpatia mama yule mtoto wake. "Mchukue mtoto huyu ukaninyonyeshee. Utanirudishia atakapokuwa mkubwa."

Ni furaha ilioje kwa Miriamu na jamaa yake! Mungu alikuwa amewasaidia katika kumtunza vyema mtoto wao.

8. Waonyeshe picha namba 61. Uliza, "Ni nini kinachofanyika katika picha hii?" Ongea kuhusu hadithi hii.
9. Rudia kifungu hiki, "Mungu yu pamoja nasi." Sasa sema pamoja na watoto.
10. Fanyeni mchezo wa hadithi hii. Chagua watoto wawe mama, baba, dada, ndugu, binti Farao na wasaidizi wake. Weka nguo katika kikapu kuwa ndiye mtoto Musa.
11. Wimbo: "Mungu yu Karibu"
12. Omba, ukimshukuru Mungu kwa ajili ya jamaa zetu.



Somo 61

# JAMAA YA MTOTO MUSA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu alitupangia tuwe na jamaa.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu yu pamoja nasi" (Isaya 8:10),

Nyimbo:
"Najua Mungu Ananitunza"
"Yesu Apenda Watoto Wote"
"Mungu yu Karibu"
"Jumapili Yenye Furaha"

Tumia picha namba 61.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Kutoka 2:1-9

Wana wa Israeli walikaa Misri kwa miaka mingi sana. Yusufu alikuwa mmoja kati ya viongozi wa nchi hiyo, lakini kwa sasa alikuwa amekufa. Wana wa Israeli nao, walifanywa watumwa wa Farao.

Mwishowe, mfalme aliamua kuua watoto wote wa kiume waliozaliwa na wanawake wa Kiebrania. Akawaamuru wazalishaji kuua watoto wote walio wavulana. Lakini wao walimwogopa Mungu na hawakutii amri hiyo ya Farao.

Mtoto mmoja alizaliwa katika jamaa ya Kiebrania (Waisraeli). Mtoto huyu aliitwa Musa. Jamaa hii ilimficha mtoto huyu nyumbani kwao kwa muda wa miezi mitatu.

Wakati ulifika ambapo jamaa hii haikuweza kumficha tena mtoto wao. Mama yake alitengeneza kisafina cha manyasi. Akakipaka lami kuzuia maji kutoingia ndani. Alimlaza mtoto ndani yake na akakiweka katika majani kando ya mto.

Bintiye Farao alikiona kisafina hicho na akasikia mtoto huyo akilia. Kifungu cha sita kinasema kwamba, "Basi akamhurumia."

Miriamu, dada yake mtoto huyo, alienda na akamleta mwanamke wa Kiebrania, ambaye ni mama yake, kumtunza mtoto huyo. Musa alipokuwa mkubwa, alipelekwa kwenda kuishi na Binti Farao.

Jamaa ni sehemu ya mpango wa Mungu. Wasaidie watoto kuelewa kwamba Mungu hutumia wazazi wao katika kuwatunza.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika. Imbeni wimbo wa "Jumapili Yenye Furaha."
2. Mwambie mtoto mmoja kupitisha kwa wenzake chombo cha sadaka.
3. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka walizotoa.
4. Ita kila jina na uweke alama katika kitabu cha rekodi.
5. Nyimbo:
   "Najua Mungu Ananitunza"
   "Yesu Apenda Watoto Wote"



moshi, meli, farasi au punda, taksi, na kadhalika. Iga mchezo jinsi kila kimoja kiendavyo.

5. Sema, "Kuna aina mbali mbali za kusafiria. Katika hadithi yetu ya leo ya Biblia, tutajifunza kuhusu mtu aliyeenda kwa safari ndefu sana. Alitumia gari luvutwalo na farasi.
6. **Fungua Biblia yako katika Matendo 8** na usimulie hadithi ya:

**FILIPO ASHUHUDIA UPENDO WA MUNGU**

Filipo alikuwa rafiki wa Yesu. Alienda kutembea katika njia itokayo Yerusalemu. Akasikia kelele za gari litembealo. Alipoangalia alimwona farasi akivuta gari fulani.

Kulikuwa na mtu ndani ya gari hilo. Alikuwa akirudi nyumbani baada ya kuhudhuria kanisa huko Yerusalemu. Humo ndani, alikuwa akijisomea Biblia ya Kuviringisha.

Filipo hakumjua mtu huyo. Alikuwa mgeni sana kwake. Filipo alienda kuongea naye alipomwona akijisomea Biblia.

"Je, unaelewa vifungu usomavyo?" Filipo akamwuliza.

"La," akamjibu. "Hata sielewi. Ninahitaji mtu wa kunisaidia. Je, waweza kunisaidia?"

Filipo aliingia katika gari lake. Akavisoma tena vifungu hivyo. Halafu akaanza kumweleza mtu huyo maana ya maandiko hayo.

"Maneno haya yanaongea kuhusu Yesu. Yesu ni Mwana wa Mungu. Mungu alimtuma Mwanawe ili awe rafiki yako. Naye Mungu anataka kuwa rafiki wa kila mtu. Anawapenda watu wote."

Mtu huyo alimsikiliza Filipo kwa makini alipokuwa akimweleza mengi kuhusu Yesu.

"Nampenda Yesu," mtu huyu akasema. "Namtaka Yesu awe rafiki yangu. Nashukuru sana kwa kuniambia habari za Yesu."

Mtu huyo aliwasimamisha farasi wake na Filipo akashuka chini. Mwishowe, aliaga mtu huyu naye akaenda zake.

Mtu huyo alipofika kwake, Kushi, naye alishiriki na wenzake maneno aliyoambiwa na Filipo. Aliwaambia watu wengi kuhusu upendo wa Mungu. Pengine aliwaambia hivi, "Nimefurahi kwa sababu Mungu anampenda kila mmoja. Nimefurahi pia kwa sababu Filipo aliniambia kuhusu upendo wa Mungu. Nimeshukuru pia kwa kupata Biblia hii yangu ya kuviringisha."

7. Wimbo: "Yesu Anipenda"
   "Nampenda Yesu"
8. Waambie watoto watengeneze barabara. Kama watoto wanasomea nje, basi waambie wachore barabara hiyo mchangani. Kama watoto hujifunzia darasani, basi wape kijisanduku kidogo au mkebe ulio na mchanga. Waambie watoto waseme kilichotendeka njiani.
9. Waonyeshe picha namba 57. Waonyeshe Filipo jinsi alivyo na yule mtu wa Kushi pia. Farasi inalivuta gari lao na yule mtu wa kushi ameshika Biblia ya kuviringisha.
10. Wimbo: "Yesu Apenda Watoto Wote"
11. Omba, ukimshukuru Mungu kwa sababu anampenda kila mmoja.



Somo la 58

# NDOTO YA YAKOBO

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu yu karibu.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Ee Bwana, Wewe U karibu" (Zaburi 119:151).

Nyimbo:
"Mungu yu Karibu"
"Najua Mungu Ananitunza"
"Yesu Anipenda"

Tumia picha namba 58.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 28

Yakobo na Esau walikuwa ndugu. Yakobo alikuwa amemdanganya Esau, na kuchukua urithi wake. Kwa hivyo Esau alimchukia Yakobo sana. Esau alipanga kumwua Yakobo wakati baba yao atakapokufa.

Rebeka, mama yao, alimshauri Yakobo. Alijua kwamba ni lazima aondoke nyumbani kwao. Isaka alimwambia Yakobo kwenda nyumbani kwa mjomba wao. Alimwambia aende kuoa msichana mmoja kati ya watoto wake. Isaka alimbariki mwanawe, Yakobo, kabla ya kuanza safari. Alimbariki jinsi alivyo barikiwa na baba yake, Ibrahimu.

Yakobo alianza safari. Wakati wa jioni alisimama ili alale. Alilala nje, na akaweka jiwe chini ya kichwa chake.

Usiku huo aliota. Alimwona Mungu akiwa amesimama karibu naye. Mungu akamwambia, "Mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako."

Soma Mwanzo 28:13-15.

Yakobo alilichukua jiwe alilolilalia na kulisimamisha kuwa mahali pa kumwabudia Mungu. Alimwabudu Mungu akiwa mahali hapo na akapaita "Betheli." Maana ya jina hili ni kusema "Nyumba ya Mungu."

Mara kwa mara, watoto huogopa wakati wa usiku. Somo hili linaweza kuwasaidia ili waelewe kwamba Mungu huwa karibu nao kila wakati. Huwatunza na kuwalinda usiku na mchana.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto.
2. Waambie watoto waweke sadaka zao katika chombo cha sadaka wanapoingia darasani.
3. Ita jina la kila mtoto na uweke alama (✓) katika kitabu cha rekodi.
4. Wimbo: "Mungu yu Karibu"
5. Sema, "Je ninyi huogopa mnapoamka usiku wakati wa giza? Wengi wetu huogopa wakati wa giza. Lakini kumbukeni **kwamba Mungu yu karibu nanyi.**



6. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema"
7. Mchezo: Fanyeni mchezo wa aina mbali za usaidizi kama; kutwanga mahindi, kupalilia mboga, kwa kumtunza mgonjwa. Waambie watoto wabahatishe kwa kusema kile ufanyacho.
8. **Fungua Biblia yako katika Matendo 9.** "Biblia inatuambia habari za mwanamke mmoja aitwaye, Dorkasi, aliyetenda mema sana. Aliwasaidia watu wengi kwa kuwatendea mema." Simulia watoto hadithi ya:

**DORKASI, MSAIDIZI MWEMA**

Dorkasi alikuwa na marafiki wengi sana. Naye alimpenda Yesu sana. Hakuwa mwanamke mchoyo bali alipenda sana kuwasaidia rafiki zake.

Aliwaona watoto ambao hawakuwa na nguo nzuri. Alitamani sana kushirikiana nao. Kwa hivyo, aliamua kuwashonea nguo.

Alichukua kitambaa na akakikata katika vijisehemu vidogo vidogo. Baadaye alichukua shindano yake na akaanza kuviunganisha na kushona nguo. Alifanya kazi kwa haraka sana. Akimaliza kushona nguo ya msichana na shati. Alishona tena suruali ndefu na shati. Alipomaliza kuzishona, aliwapa watoto hao. Kila mtu alimpenda Dorkasi kwa sababu aliwasaidia watu wote.

Siku moja, Dorkasi alishikwa na ugonjwa na akafa. Rafiki zake walihuzunika sana. Walikumbuka kwamba Petro, mhubiri, alikuwa karibu na kijiji chao. Wakawatuma watu wawili kwenda kumwita.

Petro aliandamana na watu hao hadi nyumbani kwa Dorkasi. Aliwakuta rafiki zake wakiwa wanalia na kuomboleza. Wakamwambia, "Tafadhali Petro, msaidie."

Wakamwonyesha vitu vyote alivyokuwa amewatengenezea. Halafu wakamwambia, "Amekuwa mwanamke mwema sana kwetu. Aliwashonea rafiki na jirani zake nguo nyingi sana. Alizishona kwa sababu anampenda Yesu."

Petro aliwaambia watu wote watoke chumbani humo. Akapiga magoti karibu na kitanda hicho na akaanza kuomba. Baada ya kumaliza kuomba, alisimama na kusema, "Dorkasi, amka."

Dorkasi alifumbua macho yake na akakaa kitandani. Petro alimshika mkono na akamsaidia kuinuka. Halafu akatoka nje pamoja na Petro kwenda kuwaona rafiki zake.

Watu wengi walifurahi walipomwona akiwa hai tena. Walijua kwamba Mungu alikuwa amemfufua. Hata nao wakamshukuru Mungu pamoja.

9. Waonyeshe picha namba 60. Uliza, "Ni nani aliyeko katika picha hii? Je, anafanya nini?" Waongoze watoto katika kuzungumzia yale ambayo Dorkasi aliwatendea watu, na jirani zake.
10. Wimbo: "Yesu Aliwaponya Wagonjwa"
11. Fungua Biblia yako katika 1 Petro 5:7 na usome kifungu hicho, "Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu." Rudia kifungu hicho pamoja na watoto wote.
12. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema"
13. Omba, ukimshukuru Mungu kwa kututunza na pia kwa kuwa mwema kwetu.



Somo la 60

# DORKASI, MSAIDIZI MWEMA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu alipanga tuwe na wasaidizi.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu" (1 Petro 5:7).

Nyimbo:
"Yesu Aliwaponya Wagonjwa"
"Msaidizi Nakuwa"
"Nisaidie Kuwa Mwema"

Tumia picha namba 60.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Matendo 9:36-42

Dorkasi aliishi huko Yofa. Alikuwa amemwamini Yesu Kristo. Biblia inatuambia kwamba alitumia muda wake mwingi akitenda mema na kuwasaidia maskini.

Dorkasi alishikwa na ugonjwa siku moja na akafa. Marafiki zake waliwatuma watu wawili kwenda kumtafuta Petro. Walipompata walimwambia kuwa anahitajika haraka sana.

Petro aliendа Yafa mara moja. Alipofika katika ile nyumba ambayo Dorkasi alikuwemo, aliwaona wanawake wengi walio wajane na maskini. Wengi wao walikuwa wakilia na kuomboleza. Walikuwa hawa wakikumbuka vitu vile walivyopewa na Dorkasi.

Petro aliwaambia wote watoke nje ya chumba hicho. Alipiga magoti na akaanza kuomba. Dorkasi alifumbua macho yake. Alikaa alipomwona Petro. Alikuwa ameponywa na kurudiwa na uhai wake. Habari za mwujiza huu ziliwashangaza watu sana. Hata wengi wao wakamwamini Yesu.

Njia moja ya kuonyesha upendo wa Mungu ni kwa kuwasaidia wengine. Watoto wanaweza kusaidia kwa njia tofauti tofauti. Wasaidie kuelewa kwamba jambo hili humpendeza Mungu sana.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika.
2. Sadaka: Weka chombo cha sadaka karibu na mlango ili kila mmoja aweze kuweka sadaka yake humu. Mshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka hiyo.
3. Wimbo: "Msaidizi Nakuwa"
4. Weka alama kwa majina ya wale waliohudhuria.
5. Uliza, "Je, Mungu anatutaka tuwe wasaidizi? Tunawezaje kuwa wasaidizi? Ngojea watoto wajibu.



Yeye huwatunza na kuwalinda, kwa hivyo huwa amewaondolea woga.

6. Wimbo: "Najua Mungu Ananitunza"
7. Sema, "Kuna kifungu cha Biblia ambacho kinatuambia kwamba Mungu yu Karibu. Fungua Biblia yako katika Zaburi 119:151 na usome kifungu hiki. "Ee Bwana, Wewe U karibu." Waambie watoto warudie kifungu hiki.
8. Maombi: Mshukuru Mungu kwa kuwa karibu nasi.
9. Mchezo: Waambie watoto wajifanye kuwa wamefika wakati wa usiku. Watatakiwa walale. Mtoto mmoja atakuwa mwezi. Atasimama, huku akiwa ameshika mikono yake juu ya kichwa chake. Mtoto mwingine naye atakuwa jua. Baada ya dakika chache, jua litawaamsha watoto. Sasa wataanza kufanya kazi zifanywazo wakati wa mchana.
10. Sema, "Hadithi yetu ya leo, inahusu mtu aliyelala nje wakati wa usiku." **Fungua Biblia yako katika Mwanzo 28** na usimulie hadithi ya:

**NDOTO YA YAKOBO**

"Yakobo, Yakobo," Isaka alimwita mwanawe. "Nataka uende safari ndefu sana. Nataka uende kumtembelea mjomba wako."

Yakobo alianza kujitayarisha. Alichukua nguo na chakula akaweka sandukuni. Safari hii yake ingemchukua siku nyingi sana, kwa sababu alitakiwa kutembea kwa miguu hadi kwa mjomba wake.


Muda si muda, Yakobo alianza safari yake. Alitembea na akatembea. Jua lilianza kutua na giza likawa linaingia. Yakobo aliangalia juu mbinguni, akaona nyota moja. Hatimaye, aliona nyingine na nyingine na nyingine. Usiku ulikuwa sasa umefika. "Nitaacha kuendelea na safari ili nipumzike hapa," akawaza Yakobo. Alipata jiwe zuri sana na akaliweka chini ya kichwa chake. Akalala usingizi mno.

Alipokuwa akilala, aliota ndoto. Katika ndoto hiyo aliona ngazi kubwa ikiwa imesimama juu ya nchi nayo ikielekea mbinguni. Mungu akamwambia, "Mimi nipo hapa pamoja nawe. Nitakuwa nawe kila mara. Nitakulinda kila uendako."

Yakobo aliamka, lakini hakuona mtu ye yote. Hakumsikia akisema naye tena. Lakini alijua kwamba alikuwa amesikia Mungu akisema naye.

"Mungu yu mahali hapa pamoja nami," akawaza, "Naye atakuwa pamoja nami po pote niendapo. Basi sitaogopa kamwe kwa sababu Mungu atanilinda."

11. Wimbo: "Mungu yu Karibu"
"Yesu Anipenda"
12. Watoto wanaweza kuiga hadithi hii katika mchezo. Tafuta jiwe dogo la kuweka chini ya kichwa.
13. Waonyeshe picha namba 58 na uongee kuhusu wakati wa usiku.
14. Mshukuru Mungu kwa kutulinda wakati wa usiku.



Somo 59

# DAUDI NA JONATHANI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu alitupangia tuwe na marafiki.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Rafiki hupenda siku zote" (Mithali 17:17).

Nyimbo:

"Marafiki"
"Njia ya Furaha"
"Nisaidie Kuwa Mwema"

Tumia picha namba 59.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 1 Samweli 18:1-5, 17:55-58, 20:1-17

Somo hili litakukumbusha hadithi ya Daudi na yule jitu, Goliathu. Mfalme Sauli alipendezwa sana na kijana Daudi. Akamwambia aje kuishi pamoja naye na jamaa yake.

Sauli alikuwa na mtoto wa kiume aitwaye Yonathani. Yeye na Daudi walikuwa marafiki sana. Hata waliahidiana kuwa marafiki daima.

Yonathani alimpa Daudi koti lake, upanga wake na nguo zake za vita. Wote wakawa wanajeshi. Daudi alifanywa kuwa mkuu wa majeshi kwa sababu alikuwa mwanajeshi hodari. Baadaye, Daudi alimwoa dadake Yonathani, na wote wakawa watu wa jamaa moja.

Yonathani na Daudi walikuwa marafiki maishani mwao. Hata hivyo, mfalme Sauli alianza kumchukia Daudi. Alimkasirikia pia mwanawe kwa sababu yeye alimpenda Daudi sana.

Daudi alihuzunika sana wakati Yonathani alipokufa akiwa vitani. Aliandika zaburi akieleza huzuni yake. Soma 2 Samweli 1:19-27.

Huu ni mfano wa urafiki mwema ulioelezwa katika Biblia. Mungu alitupangia ili tuwe na marafiki. Alikuwa na mpango kwetu wa kupendana na kushirikiana pamoja.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Wakaribishe watoto wanapofika. Sema, "Ninafuraha leo kumwona rafiki yangu ________." Taja jina la kila mtoto afikaye.
2. Imbeni wimbo usemao, "Njia ya Furaha" wakati watoto waendapo kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka.
3. Maombi: Omba hivi, "Asante sana Mungu, kwa sadaka tukutoleazo."
4. Rekodi: Ita jina la mtoto mmoja. Mwambie naye aite jina la mtoto mwingine. Endelea vivyo hivyo hadi watoto wote watakapoitwa majina yao. Weka alama katika kitabu cha rekodi kando ya majina ya wale waliohudhuria.
5. Mchezo: Mwalimu ataimba hivi, "Namtaka rafiki asimame nami, asimame nami, asimame nami. Nataka rafiki asimame nami. Anaitwa ________." Baadaye, wote wawili mtaimba hivi, "Tunataka rafiki asimame nasi. Anaitwa ________." Sasa mtaimba wote watatu wimbo huu. Endelea kutaja majina yao hadi watoto wote watakaposimama na kuimba pamoja nawe.
6. Maombi: Sema, "Hebu na tumshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki zetu." Omba.
7. **Fungua Biblia yako katika 1 Samweli 18** na usimulie hadithi ya:

## DAUDI NA YONATHANI

Siku moja, watu fulani walimwendea Daudi. Alikuwa akichunga kondoo wa babake. "Tumetumwa na mfalme Sauli," wakamwambia. "Anataka kukuona. Tafadhali njoo twende nawe."

Daudi alifurahi sana kwa sababu mfalme alitaka kumwona. Alienda kwa haraka hadi nyumbani kwake.

Mfalme Sauli akamwambia, "Daudi, wewe ni kijana hodari sana. Umewasaidia watu wako. Kwa hivyo, nataka uje na uishi nyumbani kwangu."

Yonathani, mwanawe mfalme, alikuwa amesimama karibu na babake. Yeye na Daudi walipendana sana. Hasa Yonathani alifurahi sana kwa sababu Daudi alitakiwa aishi pamoja nao.

Alimpa Daudi koti na upanga wake. Akamwambia, "Nakupatia zawadi hizi kwa sababu nakupenda. Nataka uwe rafiki yangu."

Daudi na Yonathani walipenda sana kuongea, kutembea na kwenda kuwinda pamoja. Wakati mwingine walicheza pamoja.

Yonathani akamwambia Daudi, "Hebu na tuapiane kuwa tutakuwa marafiki daima."

Daudi alikubali. Naye akampenda sana Yonathani. Walikuwa marafiki sana hata walipoendelea kuwa wazee. Hawakusahau ahadi yao.

Daudi alifanywa mfalme baada ya miaka mingi kupita. Daudi alihuzunika sana wakati Yonathani alipofariki akiwa vitani. Hata akandika wimbo katika Zaburi kuhusu urafiki wao.

Yonathani alikuwa na mtoto aliyekuwa kilema. Daudi alimwita na kumwambia aishi katika nyumba ya kifalme pamoja naye. Akamwambia, "Babu yako, Sauli, aliniambia niishi pamoja naye. Naye babako akawa rafiki yangu sana. Kwa hivyo, nataka wewe uje na uishi pamoja nami."

8. Wimbo: "Marafiki"
   "Nisaidie Kuwa Mwema"
9. Fungua Biblia yako katika Mithali 17:17 na usome kifungu hicho, "Rafiki hupenda siku zote." Waambie wasichana wakirudie tena, halafu wavulana nao wakiseme peke yao. Sasa waambie wote wakiseme pamoja.
10. Wimbo: "Marafiki"
11. Waonyeshe picha namba 59. Uliza, "Je, kati ya vijana hao, Daudi ni yupi? Yule kijana mwingine ni nani?
12. Ongea kuhusu mambo ambayo marafiki hufanya wakiwa pamoja. Mshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki.